



Research Article



Check for updates

Section: Literature, Linguistics & Criticism



Published in Nairobi, Kenya
by Royallite Global.

Volume 3, Issue 3, 2022

**Article Information**

Submitted: 15th March 2022

Accepted: 30th June 2022

Published: 1st July 2022

Additional information is
available at the end of the
article

<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/>

To read the paper online,
please scan this QR code

**How to Cite:**

Job, J. N. (2022). Matumizi ya jazanda katika uwasilishaji wa mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Kithaka wa Mberia. *Research Journal in African Languages*, 3(3). Retrieved from <https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/861>



Matumizi ya jazanda katika uwasilishaji wa mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Kithaka wa Mberia

Juma Nyongesa Job

Chuo Kikuu cha Pwani, Kenya

Barua Pepe: jayjuma52@yahoo.com

<https://orcid.org/0000-0001-9105-8686>

Ikisiri

Makala hii imechunguza mtindo wa jazanda na viwango vya jazanda vilivyotumika katika kusawiri mashairi yenye maudhui ya ukoloni mamboleo na uchumi. Aina mbalimbali za jazanda zimechanganuliwa kwa kuzingatia maana inayojitokeza. Mashairi ya Kezilahabi na Mberia ndiyo yamezingatiwa. Utafiti huu umezingatia uainishaji wa wataalam hawa wote ili kubaini ufanano na utofauti uliopo kintindo katika uwasilishaji wa mashairi huru ya Kezilahabi na Mberia. Nadharia ya Mtindo ilitumika katika utafiti wa kazi hii. Nadharia hii iliasisiwa na Buffon (1930) na kuendelezwa na Leech (1969). Mbinu ya usomaji wa maktabani ilitumika katika ukusanyaji wa data. Matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Utafiti huu ni muhimu kwa wanafunzi wa shule na hata kwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Makala hii inasaidia mwanafunzi kuweza kubaini aina mbalimbali ya jazanda na ishara wasilishi za jazanda.

Maneno muhimu: jazanda, Euphrase Kezilahabi, Kithaka wa Mberia, ushairi

Utangulizi

Jazanda ni kunga ya utunzi ambapo lugha inatumiwa kusawiri picha fulani kutokana na maelezo yanayotumia maneno teule au tamathali za usemi. Kwa njia hii, mtunzi anamuezesha msomaji kuona, kuhisi au kunusa kitu kinachoelezwa (Mbatia 2000). Honara (2010) anaeleza kuwa jazanda ni za aina tatu kuu: kiubia, jamii na za kibinafsia. Jazanda za kiubia ni zile ambazo zina matumizi ya dunia nzima na zinapatikana katika sehemu mbalimbali za dunia, tamaduni na wakati. Neno kama 'mama' lina matumizi mapana na likitumika kijazanda litafahamika na watu wengi. Jazanda za kijamii ni zile ambazo zimekubaliwa na jamii fulani kimatumizi au eneo fulani la kijografia. Maana ya jazanda hizi za kijamii hufungamana na jamii husika tu. Haziwezi kueleweka nje ya jamii lengwa katika uandishi ilhali za kibinafsi ni zile ambazo kila mtu anaweza kuwa na tafsiri yake na humpendeza mtu binafsi. Okwena (2013), ameanisha jazanda kulingana na rangi wanyama, mimea, miti, ndege, ndoto, harufu na kadhalika.

Muundo wa utafiti.

Utafiti huu ni wa kimaelezo ambapo maelezo kuhusu mitindo iliyotumika imetolewa. Aidha, maelezo yametolewa katika uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti.

Mahala pa utafiti

Utafiti huu ulifanyiwa maktabani. Maktaba tulizofanyia utafiti wetu ni za vyuo vikuu vya Kenyatta, Nairobi na Pwani. Maandishi na machapisho mbalimbali yalipitiwa yakiwa pamoja na vitabu vya fasihi vilivyoteuliwa kwa minajili ya mada hii. Mashairi ya watunzi Kezilahabi na Kithaka Wa Mberia yalizingatiwa. Utafiti pia ulifanywa kwenye mtandao ili kupata data inayofaa kuhusu mada hii. Aidha, tafiti za awali kuhusu ushairi na hasa mtindo katika ushairi huru zilisomwa. Kupitia kazi hizi tuliweza kupata umbali wa pengo na hata data za kutosha kujaliza pengo ambalo ni mada ya utafiti huu. Tafiti hizi pia zilisaidia katika uelewaji wa nadharia, mbinu za kukusanya data, uwasilishaji na uchanganuzi wa data ya matokeo ya utafiti.

Sampuli na mbinu za kuteua sampuli

Mashairi yaliyolengwa ni ya Euphrase Kezilahabi na Kithaka Wa Mberia. Mashairi yaliteuliwa kwa njia ya kimaksudi. Mashairi ya Kithaka yanapatikana katika nakala zake za *Msimu wa Tisa* (2007) na *Bara Jingine* (2001). Sababu na maana ni kwamba mashairi haya yametumia jazanda, taswira na takriri katika kuwasilisha ujumbe. Vilevile mashairi ya Kezilahabi katika nakala yake ya *Kichomi* (1974) na *Karibu ndani* (1988) yaliteuliwa kimaksudi kwa vile mitindo ya jazanda, taswira na takriri imetumika. Tulishughulikia diwani mbili za Kezilahabi na mashairi mbalimbali katika diwani za Kithaka Wa Mberia.

Njia na vifaa

Kazi mbalimbali zilisomwa na kuweza kuchuja kati ya zile za kufaa na zile si za kufaa. Ili kufanikisha utafiti huu tulitumia vifaa kadhaa kama tarakilishi kwa shughuli za mtandao. Kifaa hicho huwa na udhaifu kwa vile kinaweza kukwama katika ukusanyaji wa data. Kwa minajili ya kuepuka tatizo hili, tulitumia kalamu na karatasi kunakili ujumbe. Aidha, data kutokana na mashairi yaliteuliwa ilikusanywa kupitia usomaji wa kina. Kwa kusoma mashairi mitindo ilitambuliwa na kunukuliwa kisha sehemu za data tarajiwa zilibainishwa.

Uchanganuzi wa data

Data iliyokusanywa ilipangwa kwa kuzingatia vipengele vya taswira, jazanda na takriri. Kisha ikachanganuliwa kwa kuzingatia ufanano, utofauti kimatumizi, umuhimu wa matumizi ya taswira na jazanda katika uwasilishaji wa ujumbe, maswali ya utafiti, pengo la utafiti na kuongozwa na

mihimili ya nadharia.

Uwasilishaji wa data

Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kuzingatia malengo ya utafiti pia matumizi ya mifano na madondoo ya mashairi. Matokeo yaliwasilishwa katika sura sita. Mifano ya jazanda katika mashairi teule:

Jazanda za Damu

Hizi ni jazanda ambazo zina sehemu pana ya kimatumizi na zinaweza kuainishwa kama jazanda za kiubia. Shairi la Kezilahabi la *Nimechoka* na la Mberia la *Kikaoni Addis Ababa* yana matumizi haya. Shairi la *Nimechoka* (Kezilahabi 1974, uk. 34) mtunzi anasema kuwa:

*Mikono inaniuma, na waya imekwisha nikata vidole.
Damu imetiririka hadi kwapani; kujipangusa siwezi
Nimechoka. Kadiri niendeleavyo kuninginia, ndivyo... (Ubeti wa tatu)*

Damu inatambulisha machungu na ugumu ambao Waafrika wanaupitia katika maisha yao. Ni ishara ya hatari katika jamii za kiafrika. Jazanda hii inatambulisha jinsi maisha yalivyo hatarini kama wakati wa ukoloni. Jazanda ya damu inatumika na watunzi hawa wote wawili, Kezilahabi na Mberia. Matumizi haya ya damu na watunzi hawa wote ni dhahiri kuwa katika lugha kuna matumizi bayana ya maneno na ya kisanaa au yenye ukiukaji. Mhimili huu unadhihirisha matumizi tofauti sawa ya neno damu. Mberia aliangazia jazanda yake ya damu katika shairi la *Kikaoni Addis Ababa* kama kifo. Kezilahabi naye anaangazia jazanda hii ya 'damu' kama matatizo yanayowakumba Waafrika. Kwa hivyo, jazanda ya damu ya Kezilahabi na Mberia inadhihirisha matumizi sawa ya neno damu. Hili ni kwa sababu watunzi hawa wote wametumia neno 'damu' kudhihirisha masaibu yanayowasonga Waafrika.

Wakati wa ukoloni ndipo watu waliteswa jinsi mtunzi anavyoteswa katika shairi hili la *Nimechoka* (Kezilahabi 1974, uk. 34). Inadhihirisha mateso ya wakati wa ukoloni yalivyokuwa magumu kwa Waafrika. Wazungu hawakuwajali Waafrika kwa vyovyote vile. Kwa hivyo, shairi hili linatambulisha ukoloni mamboleo. Shairi hili la *Nimechoka* mtunzi anatuchorea picha ya mtu aliyepandishwa juu na kuning'inia. Anaweza kushuka chini ila kuna miti iliyochongwa inayoweza kumdunga. Waya aliyoutumia kujizuia juu umemkata vidole na damu inatiririka kwapani lakini hawezi kujipangusa.

Mtunzi katika ubeti wa pili wa shairi la *Kikaoni Addis Ababa* (Mberia 2001, uk. 2) ana matumizi zaidi ya jazanda. Mberia anaposema kuwa viongozi wa nchi huru barani Afrika walimsomea Botha kuhusu mafuvu Crossroads na damu changa Soweto. Mafuvu Crossroads ni taswira inayojenga mtindo wa jazanda kuashiria mauaji yaliyotokea kule Crossroads. Damu changa Soweto ni taswira ya kujenga jazanda ya kiubia inayoashiria mauaji ya watoto wa shule kule Soweto mwaka 1976. Kwa vile kumwagwa kwa damu ni ishara ya maafa katika jamii na inafahamika dunia nzima, basi damu ni neno ambalo huzua jazanda ya kiubia katika kazi mbalimbali za watunzi hasa kudhihirisha vifo. Watunzi wengine wanaweza kulitumia neno hili kitofauti ili kujenga jazanda za kibinafsi. Kauli hii inalingana na mhimili wa nadharia ya mtindo kuwa kazi ya fasihi hutegemea lugha, Wakati mwingine lugha ya maandishi hutofautiana. Hili hutokea kwa sababu ya uchambuzi na uhakiki wa kazi ya fasihi. Jazanda za kibinafsi hutegemea mwandishi na msomaji binafsi.

Shairi la *Hatima ya Mbu* (Mberia 2001, uk. 19) mtunzi anatambulisha usumbufu wa 'mbu' katika harakati za kufyonza damu ya binadamu. Mwandishi anatumia jazanda ya kibinafsi katika shairi hili la *Hatima ya mbu*. Matumizi ya neno 'damu' ubeti wa pili, mshororo wa nne, 'wa kunyonya watu damu'. Damu ina maana ya jasho la watu. Bidii ya watu ndio 'mbu' hutegemea akisha wanyonya

anabaki akiwasumbua kwa magonjwa na hata ukosefu wa usingizi. Magonjwa katika hali halisi ni umaskini katika nchi za Kiafrika. Kwa hivyo, matumizi ya neno damu yanadhihirika tofauti katika shairi hili, yanatoa maana ya utegemezi wala si hatari kama mashairi ya hapo awali. Hapo jazanda ya 'damu' inajitokeza kama ya kibinfsi. Mashairi haya ya *Hatima ya Mbu* na *Nimechoka* yanadhihirisha mhimili wa nadharia ya mtindo kuwa kuna matumizi bayana ya maneno na ya kisaani au yenye ukiukaji. Kwa mfano matumizi ya neno 'mbu' linakiuka maana yake ya kimsingi na kuchukuwa maana ya binadamu huku pia neno 'damu' kuashiria juhudi za kujikomboa.

Jazanda ya miiba

Miiba ni sehemu za mimea zenye ncha kali na zinazoweza kudunga. Miiba ni jazanda ya kiubia kwa vile ina matumiza mapana ya kijografia. Mtunzi katika shairi la *Afrika na Watu Wake* (Kezilahabi 1974, uk. 19) anasema kwamba kama Waafrika hawataondoa miiba iliyobaki, mgonjwa hataweka miguu yake chini na kutembea bila kujiegemeza. Ni jazanda inayoeleza athari na vikwazo vya kibepari vilivyobaki katika bara la Afrika. Mojawapo ya mihimili ya nadharia ya utafiti huu ya mtindo ni kuwa kazi ya fasihi hueleweka kwa kuchunguza lugha aliyoitumia mwandishi wa kazi hiyo. Kazi za wasanii zinaweza kueleweka kwa kuangalia na kuchunguza sifa za kazi zao. Kwa mfano, jazanda ya miiba ni jazanda ambayo watunzi wengi wa fasihi huitumia kwa sababu ya ufanano uliopo katika utamaduni wa jamii mbalimbali. Kwa kuangalia sifa za lugha za waandishi hawa utapata matumizi ya mitindo yao ina ufanana au kutofautiana. Kazi ya Kezilahabi inalingana na ya Mberia kwa matumizi ya jazanda sawia za miiba.

Kwa kawaida mgonjwa ni mtu aliye na maradhi au maumivu fulani katika mwili wake. Kwa hivyo, ni jazanda inayoeleza nchi iliyokumbwa na hali mbovu kiuchumi. Miiba iliyobaki ni ukoloni mamboleo ambao ni kikwazo kwa nchi yao kutembea bila kujiegemeza, ni usemi wenye maana ya kujitegemea kiuchumi. Matumizi ya miiba ni mojawapo ya jazanda za mimea ambazo zinajitokeza katika kazi za Kezilahabi lakini kwa vile mmea huu matumizi yake ya kimtindo yanajulikana kote duniani, unaainishwa chini ya jazanda ya kiubia.

Mtunzi katika ubeti wa pili mshororo wa kwanza, anasema kuwa 'miiba iliyomo ndani mwao lazima iondolewe upesi kabla haijaingia kati ya mifupa na kufa pamoja nao'. Mfupa ni kiungo kigumu mwilini mwa mtu au mnyama na una matumizi tofauti ya kimaana kutegemea mtunzi. Kwa hivyo, ni jazanda ya kibinafsi ambayo imejengwa na mtunzi na inaweza kueleweka tofauti na mhakiki. Mshororo wa tatu tunaambiwa na mtunzi kuwa kama hatutamtoa miiba iliyobaki mgonjwa hataweka miguu yake chini. Miiba inayotajwa ni jazanda ya kiubia. Hii ni jazanda ambayo inazua maana ya matatizo yanayolitatiza bara letu. Ingawa Waafrika walijinyakulia uhuru bado wakoloni wakongwe wanalitawala bara lao kihisia na kiuchumi. Hii ndiyo miiba anayojadili Kezilahabi na anashauri ing'olewe, yaani matatizo ya utegemezi wa kiuchumi na kutawaliwa kihisia tuyateketeze ndipo tuweze kushuhudia maendeleo barani Afrika. Mtunzi kwa kutumia jazanda hii ya miiba anafiki maelezo ya Mulokozi na Kahigi (1979, uk. 25) kuwa ushairi bora ni ule ambao una mpangilio wa maneno fasaha wenye muwala, lugha ya mkato, picha, subira na sitiari au ishara katika usemi, maandishi au mahadhi ya wimbo, ili kuelekeza wazo au mawazo. Kufunza au kueleza tukio au hisi fulani kuhusu maisha au mazingira ya binadamu, kwa njia inayogusa au mazingira ya binadamu na moyo wake.

Jazanda za wadudu

Shairi la *Kifo cha mende wekundu* (Kezilahabi 1988, uk. 33) ni mojawapo ya mashairi ambayo yana jazanda ya wadudu. Mtunzi katika ubeti wa pili anasema kwamba 'mende wataanza kutalii mipaka usiku'. Mende ni mdudu anayependa kutafuta vitu na apendaye kukaa sehemu za giza. Jazanda hii ni ya kiubia kwa vile mende ni mdudu ambaye huhusishwa na uchafu na giza katika dunia nzima. Imetumiwa na mwandishi kuwaeleza walanguzi ambao wanapenda kuendesha shughuli zao

kisirisiri ili kutapeli wenzao. Watu kama hawa huzunguka kila pembe ya nchi kwa kutumia hila na mbinu zisizoeleweka. Hawa ni watu haramu. 'Kutalii mipaka' ni usemi unaomaanisha kuzunguka nchini. 'usiku' ni taashira ya kutenda mambo faraghani au kiharamu. Mwandishi anasema kwamba 'watazuru kila pahali'. Vilevile, anakariri kwamba 'watakula walicho nacho bila uoga wala ruhusa'. Hali hii ni kielelezo cha jinsi ambavyo mataifa yaliyoendelea huyanyanyasa yale yanayostawi. Mataifa 'makubwa' yana nguvu ambazo mataifa 'machanga' hayawezi kushindana nayo. Mtunzi katika sehemu hii ametumia jazanda ya kibinafsi.

Jazanda nyingine ya wadudu inapatikana katika shairi la *Hatima ya mbu* (Mberia, 2001, uk. 19) anasema kuwa:

*Kwa mazoea machafu
Ya kuzuia watu kulala
Kwa mwenendo bughudhi
Wa kunyonya watu damu,
Wakati umekupa tuzo
Umejishindia medali (Ubeti wa pili)*

Shairi hili linazungumzia kuhusu tabia ya viongozi kukandamiza wananchi kwa kutumia mamlaka yao vibaya na kuwakosesha Waafrika amani. Kuafiki hili mshairi anatumia mtindo wa jazanda. Kwa mfano neno 'mbu' linatambulisha viongozi wenye kuwakandamiza wananchi. Mwandishi analalamikia uongozi mbaya wa viongozi wa Afrika. Waandishi hawa wawili kutumia jazanda za wadudu ni ufanano katika kazi zao. Hali hii inadhihirisha mhimili wa nadharia ya mtindo kuwa muundo wa kazi ya kubuni ndio hutumiwa na msanii katika kuifuma kazi yake. Kwa mfano, kuunganisha tukio moja na linguine, ubeti na ubeti au mshororo na mshororo. Kazi ya Mberia inaingiliana na ya Kezilahabi kwa matumizi ya jazanda za wadudu. Ni wazi kuwa mtunzi mmoja anachochea mwingine katika matumizi ya mitindo teule. Hii inadhihirika kwa jinsi wanavyotumia lugha yao.

Jazanda za wanyama

Wanyama huwakilisha maana tofauti kutegemea jamii na mtunzi. Kuna wanyama ambao maana ya majina yao rutubishi imepita mipaka ya kijamii na ni ya kiulimwengu mzima. Mnyama kama simba hutumiwa kuwakilisha mfalme katika jamii pana ya fasihi. Katika shairi la *Bara Jingine* (Mberia 2001, uk. 10) mtunzi amedhihirisha jazanda ya wanyama kwa kusema kuwa "hautakuwa ngozi ya kulinda mamba wa ikulu." Mamba ni mnyama ambaye ni hatari kwa usalama wa binadamu. Huwa na ngozi ngumu ya kumlinda dhidi ya uvamizi wa adui majini na hata ardhini. Kwa hivyo, mtunzi anatumia sifa hii, kuwatambulisha viongozi ambao ni hatari kwa usalama kwa binadamu wenzake na wakati uo huo ana "usalama wa taifa" ambao unalinganishwa na gamba la kumlinda mamba. Maudhui ya ukoloni mamboleo yanaendelezwa na mbinu hii ya jazanda katika shairi hili. Mberia anaamua kutumia jazanda za wanyama kwa vile matumizi yao ya kimtindo yanajulikana na kazi yake hufahamika kwa urahisi na hadhira lengwa. Kwa hivyo, anajikita katika matumizi ya jazanda za kiubia. Jazanda ya wanyama inatumika katika shairi la *Kumbe* (Kezilahabi 1974, uk. 36) anatambulisha matumizi haya. Kwa mfano:

*Sikilizeni, simba aliyeumizwa,
Bila haya alijiokokota kwa unyonge
Mpaka nyumbani, vidonda vikalambwa
Vikapona kwa mate ya nyumbani (Ubeti wa tatu)*

Simba aliyemizwa ni neno ambalo limetumika kijazanda kutambulisha Waafrika ambao walionekana kunawiri kushinda Waafrika wengine kwa kulaghaiwa na elimu ya Wazungu. Nyumbani linatumika kutambulisha nchi au eneo fulani ambalo lina uongozi wa Kiafrika. Vidonda ni athari zilizopatikana kwa elimu hii duni kwa jamii ya kiafrika, kisha mate ni mfumo wa kitamaduni ambao unafaa ushirikishwe katika mfumo huu wa elimu. Kwa hivyo, mtunzi anajenga jazanda ya mnyama simba ambaye ameumizwa na anamua kurudi nyumbani kutibiwa. Jazanda hii inatambulisha jinsi mfumo wa elimu wa kizungu ulivyokandamiza Waafrika. Waafrika sasa wameamua kurudi nyumbani na kujitibu kwa kutekeleza marekebisho kwa mifumo yao ya elimu.

Jazanda ambazo zinajitokeza katika shairi hili nyingi ni za kiubia. Simba ni mnyama ambaye kwa kawaida huhusishwa na ujasiri na ukali, kwa hivyo Kezilahabi anatumia jazanda ambayo inafahamika zaidi. Hali kadhalika neno kidonda linatumika kwingi duniani. Jazanda hizi za kiubia huibusha maana fulani mahususi. Mfano ambao unaweza kutumiwa kudhihirisha hili duniani ni matumizi ya rangi. Rangi nyeupe huwakilisha amani na nyekundu hatari. Kwa hivyo, mtunzi anaweza kuathiriwa na jamii yake katika matumizi ya jazanda au kuathiriwa na jamii pana ya dunia. Muundo wa kazi ya kubuni ndio hutumiwa na msaani kutoa ujumbe wake. Kezilahabi anatumia samba kuumba ujumbe wake ili aweze kueleweka. Simba anatumia tuelewe ujumbe wa Kezilahabi. Mtunzi hutumia jazanda, taswira na thamatali zingine za lugha ili kuvutia hisia na mguso wa namna ya ajabu katika moyo wa msomaji. Hisi ambazo huibuliwa wakati mwingine hutegemea mtunzi na mhakiki wa kazi hiyo. Hapo ndipo upekee wa mtunzi hujitokeza hasa kwa uteuzi wake wa maneno na mtindo kwa jumla.

Kezilahabi amedhihirisha kwamba mfumo wa ukoloni mamboleo umejaa ubandia na ahadi za uongo za uhuru, demokrasia, umoja, haki, usawa na ushirikiano. Anaafiki hili kwa kutumia jazanda ambazo zina maana lengwa au za kiubia. Mara nyingi jazanda hizi mtunzi huwa tayari ameunda kisa kisha hukitiririsha kwa jazanda mahususi.

Katika shairi la *Mafahali Wapigana* Kezilahabi (1974, uk. 6) mtunzi anaonyesha mzozo baina ya viongozi huku raia wakishangilia bila kuelewa kinachoendelea. Mtunzi anajenga makundi mawili shupavu ambayo anayalinganisha na fahali. Katika ubeti wa kwanza mtunzi anasema kuwa "mafahali wenye matumbo wanapigana." Jazanda hii inaashiria kuwa watu wenye madaraka makuu wanazozana. "Matumbo" ni jazanda ya mali au ukuu. Hii ina maana kuwa wanachozozania viongozi ni suala la umilki wa mali.

Jazanda za ndege

Ndege wa mbuga na wa nyumbani hutumiwa kutambulisha maana tofauti. Ndege kama njiwa hutumiwa duniani kutambulisha amani, mbuni katika jamii za kiafrika hutambulisha hatari na milio ya ndege asubuhi na mapema ni ishara ya siku njema kuanza. Katika diwani ya Bara Jingine Mberia anatumia kuku aina ya jogoo kutambulisha watawala wa Kiafrika. Shairi la *Bara Jingine* (Mberia 2001, uk. 19) mtunzi anatumia kiwango hiki cha jazanda. Kwa mfano:

*Kusini mwa Limpopo
Melan na kisiwa cha Robben
Sasa ni mambo ya jana
Lakini katika Ekweta
Maghala na familia
Zinatafunwa na miako
Kusudi kusaidia jogoo
Kuendelea kuwika (Ubeti wa 2)*

Kusaidia jogoo kuendelea kuwika ni jazanda inayoashiria kuwa watu wanaopinga viongozi huteketezwa ili viongozi walio mamlakani wazidi kuongoza. Huu ni ukoloni mamboleo kwa bara letu la Afrika. Jogoo ametumika kijazanda kuashiria viongozi ambao wamo katika hatamu za uongozi na ni madikteta katika uongozi wao. Jogoo ni jazanda ya kijamii kwa vile matumizi yake yanafahamika katika jamii zinazofuga kuku. Jazanda hii ikitumiwa katika jamii ambazo hazifugi kuku itakuwa ngumu kwa jamii hizo kufahamu maana ya neno hili. Kwa hivyo, mshairi anatumia ndege kutambulisha jazanda ya kijamii. Hili pia ni wazi kuwa msanii huathiriwa na mandhari anamokulia katika uandhishi wake. Hasa kwa mali ghafi anayotumia kwa kazi yake.

Jazanda za sehemu za mwili wa binadamu

Kuna matumizi ya vichwa kama sehemu ya mwili wa binadamu kijazanda katika shairi la *Nimechoka* (Kezilahabi 1974, uk. 34) anatumia jazanda hizi za sehemu za mwili wa binadamu. Kwa mfano:

*“Kichwa kimoja kinasema kwa sauti
Mnaliona Hilo!”*

Kichwa kimetumika kutambulisha wanadamu ambao wamekataa kujitambulisha na mshairi. Kwa hili mshairi anatambulisha jinsi ulimwengu umejawa na usaliti. Matumizi mengine ya jazanda za sehemu za mwili wa binadamu yanajitokeza katika shairi la *Hatumuoni* (Kezilahabi 1988, uk. 31). Mtunzi anasema kuwa ‘walio mbele ni warefu tulio nyuma mbele hatuoni. Hatutaki vyenu visogo vichafu kuona, kochi chini’. Taswira ya viongozi kuwa warefu na hivyo kuwazuia walio nyuma kuona mbele ni jazanda inayoashiria kuwa viongozi ndio vikwazo au vizuizi kwa wananchi. Aidha, kuna jazanda ambayo imejengeka katika visogo vichafu vya viongozi. Kisogo aghalabu ni sehemu ya nyuma ya kichwa cha mtu. Unaweza kuona kisogo cha mtu ukiwa nyuma yake. Hii basi inaashiria kuwa wale wanaoongozwa wamechoshwa na matendo machafu ya viongozi. Jazanda hii inaashiria kuwa matendo ya viongozi hawa ni machafu na yasiyofaa. ‘Kochi chini’ ni msemu unaojenga jazanda inayoashiria kuwa viongozi walio mamlakani wakati huo hawafai na kwa hivyo wanafaa kung’atuka mamlakani. Jazanda hizi zinaainishwa kama za kiubia kwa matumizi yake ya mapana. Mtunzi anasema kuwa:

*Acheni acheni kelele, kelele za jaza-tumbo
Uongozi umewapaka rangi
Madaraka yamewalevya ninyi
Mwanza maneno! (Ubeti wa 1)*

Taswira ya kelele za jaza-tumbo ni msemu na unaashiria kuwa viongozi wanapiga tu kelele za kuendeleza maslahi yao kibinafsi. Taswira ya viongozi kuwapaka rangi na madaraka kuwalevya uongozini ni msemu na inaashiria kuwa viongozi wamebadilika mienendo na sasa wanajali maslahi yao tu ya kibinafsi bila kuwajali wananchi. Yaani viongozi wanatumia mamlaka vibaya. Mtunzi anaendelea kusema: twataka chagua watu, watu, watu. Jazanda hii ya kuchagua watu inaashiria kuwa mienendo ya viongozi ni ya kihawayani ndiposa wananchi wanataka kuchagua viongozi wenye utu. Jazanda ya viongozi kuwa walevi inaashiria kuwa mienendo ya viongozi ni mibaya mno. Hii ndio sababu Kezilahabi anawashauri kwamba wayavue madaraka hayo na kuwapisha wenye nia.

Shairi la *Mafahali Wapigana* (Kezilahabi 1974, uk. 5) katika ubeti wa kwanza mtunzi anasema kuwa ‘baada ya vumbi kuisha, mshindwa alikuwa amekwisha kimbiba, huku mshindi juu ya kichuguu amekaa akionyesha kidole kimoja sasa’. Hii ni jazanda na inaashiria kuwa baada ya mzozo ulioshuhudiwa na wananchi kuisha, mshindi alikuwa ameshikilia uongozi wa nchi huku akionyesha

ishara ya umoja. Kidole kimoja ni jazanda ya umoja bila kujali hali halisi ya umma. Huu ni wito wa kinafiki wa viongozi wengi wa kiafrika wanaojali tu ukuu na maslahi ya kibinafsi, hawasemi ukweli. Anaendelea kusema kuwa:

*Kilikuwa kivumbi hicho.
Sasa pahali hapo pametulia tuli,
Ambapo kutembeza midomo ndo kusikika
Kunyamaza ndo basi kudhaniwa.
Patulivu! Patulivu! Patulivu kweli! (Ubeti wa pili)*

‘Kutembea midomo’ ni jazanda yenye maana ya kuongea kuhusu uongozi wa kimabavu ambao haupendezi viongozi.

Jazanda za vitu ambavyo havina uhai

Kichwa cha shairi la Ngoma ya Kimya Kezilahabi (1988, uk. 4) ni jazanda inayoongoza ujumbe wa shairi zima. Ngoma kwa kawaida ni mchezo wa kufuata mdundo wa ala fulani. Kwa hivyo, wacheza ngoma ni jazanda inayoeleza dhana ya wakoloni walionyonya nchi kulingana na mfumo wa kibepari usiojali maslahi ya umma. Uwanja uliokauka majani ni jazanda inayoashiria uchumi wa nchi ambayo iliathiriwa mno na ubepari wa ukoloni mamboleo. Njuga ni kengele ndogo ndogo zifungwazo miguuni, mikononi au shingoni wakati wa kucheza ngoma. Manyonya na kindu pia huvaliwa wakati wa kucheza ngoma. Ni mabaki ya athari baada ya ubepari wa kikoloni. Wachezaji waliozidisha mbwembwe ni jazanda yenye maana kwamba wakoloni walijaa majivuno. Katika sehemu hii mitindo imejengana, jazanda inajitokeza kupitia kwa taswira ya maelezo ambayo iko dhahiri. Jazanda hii inatumia wanadamu na vitu ambavyo havina uhai lakini vina maana fulani kifasahi. Ili maana hii ijitokeza vitu hivi vinapachikwa maana tofauti kuwakilisha ujumbe wa mshairi. Kwa mfano mabawa yanayotumika wakati wa kucheza ngoma yanahamishiwa maana ya mabaki ya ukoloni mkongwe kwa nchi za Afrika.

Mtunzi katika ubeti wa kwanza anaeleza kuwa ‘wacheza ngoma wamekwishaondoka na kilichobaki ni uwanja uliokauka majani, njuga, manjonya na kindu zilizondondoka toka kwa wachezaji waliozidisha mbwembwe nao watazamaji wakipiga kelele na vigelegele’. Mtunzi ametumia jazanda ya watazamaji akimaanisha Waafrika ambao amewatweza kwa kushangilia tendo hilo kwa kukosa kuelewa. Amewabeza kwa kupiga kelele na vigelegele kushangilia “uhuru” kwani hawaelewi kuwa ni uhuru wa bendera tu. Kwa hivyo, mtunzi anaonyesha kuwa uhuru waliopata haufai chochote. Unyonyaji utaendelea, Kezilahabi anasema kwamba ‘ni jana tu walikuwa hapa’. Usemi huu una maana kuwa si muda mrefu uliopita tangu wakoloni wakongwe wawe nchini Tanzania. Hali kadhalika, anaeleza kwamba ‘wachezaji sasa wanafikira ngoma ijayo’. Taashira hii inamaanisha kwamba wakoloni sasa wanafikiria mbinu nyingine za kutumia ili kuzidi kunyonya uchumi wa Tanzania, hasa kudumisha ukoloni mamboleo.

Mtunzi anakiri kwamba “watazamaji” hawayakumbuki maneno ya nyimbo zote zilizoimbwa. Jazanda hii ina maana kwamba Waafrika hawaelewi hulka zote za matendo ya kikoloni. Hii ndiyo sababu anatumia msemu kwamba zilizobaki ni taswira hai na vivuli. Hii inadhihirisha kwamba Waafrika wanaona athari za matendo ya kikoloni lakini kuna ukungu wa ujinga unaowafanya kukosa kuelewa uhalali wa mambo. Hawaelewi hila zitumikazo na mienendo ya wakoloni mamboleo.

Mtunzi katika ubeti wa pili, anasema kwamba ‘labda miti hii michache yakumbuka.’ Miti michache ni jazanda ya kibinafsi, inawakilisha watu wachache ambao wanaweza kung’amua sera ya kikoloni. Anaendelea kusema kwamba ‘ataviokota’ atengeneze vazi lake. Usemi huu una maana kwamba atakusanya vilivyoachwa na wakoloni mamboleo ili kujijenga kiuchumi. Hii ndiyo sababu mtunzi anasema kwamba ‘kisha atacheza ngoma yake kimyakimya katika uwanja huo mpana

ulioachwa wazi bila watazamaji'. Hapa ananua kujiendeleza kisirisiri katika mfumo wa kiuchumi ulio tupu bila chochote.

Mtunzi anaashiria jazanda anaposema kwamba 'upepo utamfundisha lugha ya kimya maana yule mwanamke amekwisha jifungua.' Mwanamke ambaye anazungumziwa hapa si mwingine ila ni viongozi ambao walikuwa wamepanga kuongoza kwa kiimla na ubinafsi nchi ya Tanzania. Kwa hivyo, Kezilahabi ametumia jazanda ya vitu visivyo na uhai kuwabeza wale watu walionua kuwaongoza kwa ubinafsi na kujinufaisha wao wenyewe katika mfumo wa kijamaa. Matendo kama hayo yanaashiria viongozi ambao ni nguzo ya ukoloni mamboleo katika Afrika huru. Huu ni mfumo wa viongozi waliojitenga na umma ili washirikiane na waendeleze ubepari kuzidi kuwanyonya na kuwagandamiza wananchi wa tabaka la chini. Ni viongozi kama hawa ambao hasa wanasaliti uhuru wa nchi zao. Hawajali maslahi ya umma bali ubinafsi unawafanya kuwa vikaragosi wanaohudumia 'mabwana' wao kutoka nje. Viongozi kama hawa hawawezi kamwe kuhudumia vyema watu wanaowaongoza. Kwa sababu ya ubinafsi wa kucheza ngoma ya kimya, huwa hawana mawasiliano mema na jamii wanazohudumia. Kwa hivyo, huzuka dhuluma na unyanyasaji wa umma.

Honara (2010), anasema kuwa kuna jazanda za kawaida kama njiwa huwakilisha amani, rangi nyekundi huwakilisha hatari au mapenzi na nyeusi huwakilisha matendo mabaya ya kisiri. Kwa hivyo, hizi ndizo baadhi ya jazanda za kiubia ambazo zinajulikana kipana. Mtunzi katika shairi la *Chai ya jioni* ubeti wa kwanza, anatumia jazanda ya kujenga nyumba kueleza juhudi za kujenga taifa. Ameonyesha kwamba katika harakati za kujenga nyumba itabidi jasho likuoshe. Jazanda hii ina maana kwamba ni kazi ngumu ambayo ni kutoa jasho jingi. Vilevile ametumia jazanda ya kimatendo au kiishara ya kufyeka, kupima na kuweka nguzo, paa na kadhalika kueleza kazi ya ujenzi wa nyumba. Hizi juhudi ni sawa na kujenga taifa kwani kiongozi hutokwa na jasho jingi. Kufyeka ni jazanda ya kuondoa vikwazo vya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Pia lazima afanye makadirio ya kitaifa katika idara mbalimbali na kuteua wasimamizi bora ambao watakuwa ndio nguzo ya taifa. Huu ndio ujumbe uliojikita katika ishara ya kupima na kuweka nguzo. Usimamizi bora ni tegemeo na mhimili wa taifa. Aidha, ametumia jazanda ya kuweka paa na kukandika kueleza dhana ya viungo vitakavyositiri taifa kama vile idara ya ulinzi, elimu, afya, kilimo miongoni mwa nyingine. Baada ya kufanya hayo yote, mtunzi anaeleza kwamba siku nyingi hazitapita kabla hujaingia na mgeni. Usemi huu una maana kwamba utatembelewa na mgeni asiye na mwaliko.

Tumekwishaona kupitia kwa mashairi hapo awali ya utafiti huu kuwa maudhui peke yake hayawezi kuunda kitu ambacho ninaweza kukiita ushairi; na kwamba ili ushairi uweze kupata sura yake, sanaa au fani ni lazima ichukue sehemu kubwa. Mtunzi katika shairi la *Kitini* (Mberia 2007, uk. 21) anazungumzia kuhusu viongozi wa kiimla na wasiojali maslahi ya wananchi wanavyopiga chenga na kubaki mamlakani. Huko kutojali ndiko kunatambulisha ukoloni mamboleo kwenye ubeti wa kwanza mshairi anasema kwamba walichoshwa misuli kwa kupambana na dhiki ya miongo miwili. Dhiki hizi ni mateso ambayo Waafrika walikuwa wakipitia kwa sababu ya uongozi mbaya. Mtunzi anasema kwamba waziri aliyepata malalamiko yao aliwadhihaki kwa kusema kuwa "juhudi zenu zenye nia ya kung'oa chama". Kung'oa chama imetumika kama jazanda ya kung'oa uongozi. Jazanda ya chama imetumika kama hali ya kung'oa uongozi.

Jazanda pia inajitokeza katika ubeti wa pili. Mtunzi anasema kwamba "alipotanabahi kuwa chombo chake kilikuwa taabani". Ukweli ni kuwa siasa mbaya ni ya kutumia na kutupa jaani. Neno "chombo" lina maana ya uongozi. Uongozi wake unalinganishwa na chombo ambacho kwa kawaida ni kama kifaa.

Jazanda inajitokeza hasa katika matumizi ya msemu kutupa jaani. Kwa kawaida kutupa jaani ni kutupilia mbali jambo ambalo halina maana. Jazanda hii ni ya kiubia kwa vile inatumia ishara ya kutupa kitu jaani na kila jamii ina hali hii ya kutupa taka. Kitendo hiki kinaonekana wazi na ni msemu katika jamii ya Waswahili. Maudhui ya ukoloni mamboleo yanaendelezwa na mbinu hii ya jazanda. Hasa kwa vile Waafrika walikuwa wakitumiwa na wazungu wakati wa ukoloni. Baada ya

kutumiwa kutesa Waafrika wengine walikuwa wakitupiliwa mbali. Kwa hivyo, uongozi wa sasa unatumia wananchi wengine kuwatesa wengine kisha kuwatupila mbali.

Jazanda ipo kwa matumizi ya neno kiu. Kiu ni neno ambalo hutumika kuashiria ile hamu ya mtu kuwa nayo ili kupata maji ya kunywa (kukata kiu ya maji). Lakini katika ubeti wa tatu mshairi anazungumzia kiu ya uhuru wa Waafrika. Kwamba Waafrika walikuwa na hamu ya kupata ukombozi na uhuru wenye haki kamili.

Jazanda za maneno teule

Watunzi hutofautiana katika matumizi ya maneno, kuna maneno ambayo yanaweza kutumika na kutambulisha jazanda. Maneno haya wakati mwingine hulingana na jamii. Neno kama 'baba' lina matumizi mapana kushinda matumizi yake ya kimsingi. Mtunzi katika Shairi la *Nimechoka* (Kezilahabi 1974:32) anazungumzia kuhusu 'juu' ambapo amefungwa. Juu anayoizungumzia ni ugumu wa maisha unaomkabili. Neno hili 'juu' linapata maana tofauti na kuwa na maana ya ugumu wa maisha, mtindo huu unatambulika kama jazanda ya kibinafsi. Maisha yamekuwa magumu kwa sababu ya viongozi wabaya. Uongozi ambao umo mamlakani haujali raia. Ndiposa mwandishi anasema kuwa 'sauti ya baba inasema kwa msisitizo najua utafika wakati itakulazimu kudondoka'. Baba ambaye anarejelewa ni jazanda ya kiubia kuashiria kiongozi wa taifa ambaye hajali Waafrika wenzake. Neno 'baba' limetumika katika hali ya kutambulisha kiongozi wa wananchi. Katika fasihi hutumika vivyo hivyo kama kiongozi. Hali hii inawiana na mhili wa nadharia ya mtindo kuwa katika lugha kuna matumizi bayana ya maneno na ya kisani au yenye ukiukaji. Neno baba linakiuka matumizi yake ya kawaida ya mzazi wa kiume.

Shairi hili pia linaendeleza jazanda nyingine, mtunzi anatumia maneno 'ncha za waya' kijazanda. Ncha za waya ni ugumu wa maisha. Kwamba gharama ya maisha imekuwa ngumu kwa mwananchi wa kawaida na kwa hivyo amechoka. Mbinu hii ya jazanda inaendelezwa hasa mshairi anaposema kwamba "chini yake anaona miti iliyochongwa ikifuata usawa wa waya". Miti hii ni ugumu wa maisha ambao unaongozwa katika nchi ya mtunzi. Maisha yanaendelea kuwa magumu kwa mtunzi na anamua kusalimu amri.

Shairi la *Kifo cha Mende Wekundu* linatumia maneno 'makubwa' na 'machanga' kuwasilisha mtindo wa jazanda. Honara (2010) anaeleza jazanda kama kitu kuchukua maana nyingine tofauti. Kwa hivyo, mataifa ambayo yanawiri kiuchumi yanatambuliwa kama mataifa makubwa na ilihali yale ambayo hayajaendelea kiuchumi yanatambuliwa kama 'machanga'. Hii ndiyo sababu ya mataifa 'makubwa' kutenda lolote bila kujali. Mwandishi anaeleza kwamba masalio yatakuwa ndiyo ajira ya kazi yako. Usemi huu unaeleza dhana kwamba watu kama hao watanyakua kila kitu chenye thamani. Kitakachoachwa ndiyo mshahara wa kazi ngumu ya kujenga taifa lako. Mtunzi anabainisha kwamba mataifa machanga yamefanywa fukara kulingana na sera kama hii. Hii ndiyo sababu yameendelea kutegemea mikopo na misaada kutoka nchi zilizostawi. Huu ukosefu wa uwezo ndiyo njia moja ya kurutubisha ukoloni mamboleo na kunyanyaswa.

Shairi la *Obasanjo* (Mberia 2001, uk. 19) mtunzi ametumia shairi hili kusifia kuondoka mamlakani kwa hiari kwa Olusegun Obasanjo aliyekuwa Rais wa Nigeria. Tazama vile anavyotambulisha hili:

Olusegun Obasanjo
Naujenga huu mnara
Uwe ukumbusho wako (Ubeti wa 1)

Kitendo cha Olusegun Obasanjo kinastahili sifa kwani katika bara la Afrika viongozi hawaondoki mamlakani kwa hiari. Ni kama wakoloni walivyokuwa, ililazimu waondolewe kwa nguvu. Katika kujenga maudhui ya ukoloni mamboleo mwandishi alitumia mitindo ya jazanda za vitu ambavyo havina uhai. Mnara hujengwa kama ukumbusho wa watu au matendo muhimu

maishani. Mtunzi anaposema naujenga mnara huu uwe ukumbusho wako, ni jazanda inayoashiria kuwa shairi alilitunga kwa heshima ya Obasanjo. Jazanda hii inatambulisha mazuri yote ambayo yalifanywa na Obasanjo. Jazanda hii ni ya kijamii kwa vile inafahamika na watu wachache ambao wanamfahamu Obasanjo.

Mtunzi katika ubeti wa pili, anatumia jazanda anaposema kuwa kitendo cha Obasanjo kilikuwa na ladha kama matone ya asali katika ulimi ambao umezoea kumumunya pamba- kama tujuavyo asali ni tamu sana na pamba nayo haina ladha yoyote. Honara (2010), ili kujenga jazanda mwandishi huishia kutumia mbinu zingine za lugha kama tashbihi. Mtunzi katika shairi hili la *Kikaoni Addis Ababa* anatumia tashbihi kujenga jazanda ya kiubia. Jazanda hii ya tashbihi inaashiria kuwa kuondoka mamlakani kwa hiari kwa Obasanjo kilikuwa kitendo kizuri ajabu na cha kuvutia katika bara ambapo viongozi hawakuondoka mamlakani kwa hiari. Mtunzi anatumia kitendo hiki cha Obasanjo kuwakebehi viongozi wengine katika nchi za Kiafrika. Kwa mfano katika ubeti wa tatu, mtunzi anasema 'Obasanjo alikuwa kileleni mithili ya mwewe juu ya mparamuzi'. Jazanda ya kuwa kwenye kiti ni kuwa kiongozi au Rais wa nchi ya Nigeria. Mtunzi katika ubeti wa nne, anasema kuwa mikononi alikuwa na bunduki, kichwani akili au ujuzi, lakini badala ya kushikilia kifayatulio kama onyo kali kwa wananchi, Obasanjo aliinua mkono wa kwaheri na kwa hiari akateremka kutoka kiti cha enzi. Hali hii ya kimaelezo na ya kuona, inaashiria kuwa licha ya Obasanjo kuwa na akili na ujuzi mwingi na pia kuwa na uwezo wa kutumia bunduki au wanajeshi ili aendelee kuning'inia mamlakani, hakufanya hivyo. Badala yake aliwaaga na kung'atuka kutoka mamlakani kwa hiari. Kuinua mkono ni ishara ambayo inafahamika na jamii pana kama ishara ya kwaheri. Hii ni kwa sababu ya mwingiliano wa jamii. Mhimili mmoja wa nadharia ya mtindo ni kuwa kazi ya fasihi inaweza kueleweka tu kwa kutegemea kuhakiki na kuchunguza lugha iliyotumika. Mtunzi katika ubeti wa tano anasema:

*Katika bara ambapo
Wapandao vitini
Hawashuki.*

Wapandao vitini kutoshuka ni jazanda inayoashiria kuwa barani Afrika viongozi hawaachi hatamu za uongozi kwa hiari. Anaendelea kusema kuwa:

*...Isipokuwa mikono ya mauti
Iwapende, iwachukue
Au cheche za fataki
Zilipuliwe na askari
Chinii ya makalio yao
Nuru ya kitendo chako
Inastahili mnara (Ubeti wa 5)*

Mikono ya mauti iwapende na iwachukue ni taswira inayoashiria kuwa viongozi hawaondoki mamlakani kwa hiari ila tu wafe kifo cha kawaida wakiwa bado uongozini. Cheche za fataki zilipuliwe na askari chini ya makalio yao, ni jazanda ya kibinafsi. Inayoashiria kung'olewa mamlakani kwa nguvu hasa kwa kutumia silaha. Mtunzi kusema kuwa 'nuru ya kitendo chako inastahili mnara' ni jazanda inayoashiria kuwa kuondoka mamlakani kwa hiari kwa Obasanjo ni kitendo cha heshima.

Kiishilio

Makala hii imezingatia usawiri wa maudhui ya ukoloni mamboleo na kiuchumi kwa kupitia mtindo wa jazanda ambao umeangaziwa zaidi. Mashairi yaliyochanganuliwa yamedhihirisha kuwa watunzi

hutumia jazanda mbalimbali kiufundi ili kujenga maudhui. Mtindo unaakisi njia ya mwandishi au msanii anayehusika katika kuyatazama masuala fulani, ni njia ya kuiwasilisha na kuifumbata tajriba yake, kuupanga na kuwasilisha welewa au ung'amuzi wake wa jamii. Viwango vya mitindo ya jazanda vilizingatiwa. Watunzi hawa wote walitumia mtindo wa jazanda katika mashairi yao. Viwango mbalimbali vya jazanda vilijitokeza katika mashairi ya watunzi hawa. Hali kadhalika, kuna baadhi ya viwango ambavyo waliwiana kimatumizi katika kazi zao. Viwango kama vya jazanda za damu, jazanda za wanyama na jazanda za maneno teule vina ufanano wa matumizi ya kimtindo. Aidha, waliwiana kwa matumizi ya jazanda za kiubia na kijamii. Wote waliishia kutumia jazanda za maneno teule ambayo matumizi yake yanatambulika pakubwa lakini katika viwango vya jazanda za vitu ambavyo havina uhai, sehemu za mwili wa binadamu na jazanda za kibinafsi walitofautiana kimatumizi. Sura inayofuata imeshughulikia takriri kwa mashairi yanayohusu masuala ya kiuchumi na ukoloni mamboleo.

Marejeleo

- Allen, G. 2000. *Intertextuality*: New York: Routledge 29 West 35th Street.
- Arnold, M. 1849. *The strayed Reveller and other Poems*. Fellowers; Ludgate Street.
- Babusa, H.O. 2005. *Vigezo badalia kuhusu uainishaji wa mashairi ya Kiswahili*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Bakhtin, M. 1981. *Theory of the text*. London: Routledge.
- Coombes, H. 1953. *Literature and Criticism*. London: Chatto and Windus.
- Culler, J. 1982. *The Pursuit of signs*. London: Rotledge and Kegan Paul.
- Hartman, C, 1980. *Free Verse: An essay on prosody*. London: Princeton University Press Atlanta
- Heidigger, M. 1971. *Poetry, Language and Thought*. New York: Haper and Row publishers
- Honora, F. na S. Susan 2012. *The reporter Who died Probing*. Washington: Amazon.
- Indede, F. N. 2008. *Mabadiliko katika umbo la ushairi na athari zake katika ushairi wa kiswahili*. *Swahili Forum* no. 15 (uk73-94).
- Kahigi, K.K na Mulokozi, M. M. 1982. *Kunga za ushairi na Diwani ya Yetu*. Daressalam. Tanzania Publishing House.
- Kezilahabi, E. 1973. *The Development of Swahili Poetry: 18th-20th Century*. Kiswahili Juzuu 42/2. TUKI, Chuo Kikuu Cha Dar es salaam.
- Kezilabi, E. 1974. *Kichomi*. London: Heineman.
- Kezilahabi, E. 1988. *Karibu ndani*. Dar es salaam: University Press.
- Kiango, J. G 2005. *Special Surveoy Article: African Asia* no. 5 (uk 157-166).
- Kimani, R. 1989. *Nguzo za ushairi wa Kiswahili*. Nairobi: Macmillan Kenya
- King'ei, K na Amata, K. 2001. *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi. Acaccia Stntex Publishers.
- Kingei, K. na Kisovi M. 2005. *Msingi Wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: K. L. B.
- Kuhenga, C. 1977. *Tamathali za usemi*. Dar es Salaam: East Africa Literature Bureau.
- Leech, G. 1969. *A linguistic Guide to English Poetry*. London. Longman.
- Leech, G. 2008. *Language in Literature*. London. Pearson Education Limited. M. A. Chuo Kikuu Cha Kenyatta.
- Masinde, E. 1992. *Mitindo katika mashairi huru*. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Cha Kenyatta (Haijachapishwa).
- Masinde, E. 2003. *Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui*. Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Mbatia, M. 2000. *Mwanadamu na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mberia, K, 2007. *Msimu Wa Tisa*. Nairobi: Marimba Publication.
- Mberia, K. 2001. *Bara Jingine*. Nairobi: Marimba Publication.
- Mlokozi, M. M. 1995. *History of Kiswahili poetry*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.
- Mlokozi, M. M. 1996. *Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili*. Daresalaam: TUKI.
- Mohamed, S. A. 1995. *Kunga za nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*: East African Educational Publishers Ltd.
- Momanyi, C. 1991. *Matumizi ya Taswira kama kielelezo cha uhalisi katika utenzi wa Al-Inkishafi*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Msokile, M. 1993. *Misingi ya uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East Africa Education Publishers
- Ndumbu M. J. 2011. *Matumizi ya Takriri na Sitiari Katika Uteuzi wa Rasttlghuli*. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Ndungo C.M. na Wafula, R.M. 1993. *Nadharia ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: University of Nairobi Press.
- Ndungo, C. M 2006. *The image of women in Afrika oral literature. A case study of Gikuyu oral literature*. Gender issues Research Report Sereis, No. 23. (Uk 19-24)
- Ndwiga, P. N. 2013. *Mitindo Katika Mashairi ya Diwani ya Karne Mpya*. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

- Njogu, K. na Chimera, R. 1999. *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Okwena, S. 2013. *Matumizi ya jazanda katika tamthilia tatu za Timothy Arege*. Tasnifu ya kufuzu cheti cha uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Oyoyo, J. O. 2013. *Uhakiki katika ngano tano za Kiswahili*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Ruo, K. K. 1989. *Nguzo za ushairi*. Nairobi: Macmillan.
- Simpson, P. 2004. *Stylistic: A Resource book for Students*. London: Routledge.
- Senkoro, F. E. M. K. 1988. *Ushairi Nadharia na Tahakiki*. Dar es salaam: Press and Publicity.
- Senkoro, F. E. M. K. 1982. *Fasihi*. Dar-es - salaam: Press and Publicity center.
- Simuyu F. W. 2011. *Kitovu cha Fasihi Simulizi: kwa shule, vyuo na ndaiki*. Mwanza. Serengeti Bookshop.
- TUKI 2004. *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Wafula, R.M. 1992. *Nadharia kama mwongozo wa utunzi na uhakiki katika fasihi*. Makala ya Semina Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Wafula, R. na Njogu, K. 2007. *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Nairobi. Routledge publishers.
- Wambua, M. 2001. *Mtindo wa nyimbo za Kakai Kilonzo*.Tasnifu ya M. A Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Wamitala K. W. 2003. *Kamusi ya Fasihi: Stilahi na nadharia*. Nairobi: Nairobi Focus.
- Wamitila K. W. 2003. *Kichocheo cha Fasihi na Andishi*. Nairobi: Nairobi Focus.
- Wamitila K. W. 2008. *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa.
- Wamtila, K. W. 2002. *Uhakikiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix
- Wanyama, A. 2006. *Maudhui na mtindo katika utendi wa wabukusu Khusala Kamuse*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Wekesa, A. 2008. *Matumizi ya taswira katika ushairi-huru wa Kiswahili*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Wellek, R. and A. Warren, 1949. *Theory of Literature*. London. Penguin Books, Harmondsworth.
- Yule, G. 1986. *The study of Language*. New York: Cambridge University Press.